

akaunti Na. 9932445461 (inayotumia Dola za kimarekani – US \$ Account) kwa jina la GPSA – UNUNUZI WA MAGARI KWA PAMOJA COLLECTION ACCOUNT iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

Mara tu baada ya kuhamisha fedha hizo ni muhimu kuwasilisha nakala za nyaraka za uhamisho wa fedha hizo kwa Mtendaji Mkuu wa GPSA, S.L.P 9150, DSM au Simu Na.022-2866071/2861617 au kwa barua pepe: ceo@gpsa.go.tz



iv. Kupata magari yanayolingana na viwango vya ubora vilivyowekwa kutokana na kutumia wataalam waliobobea katika kufanya ununuzi na ukaguzi.

v. Kuwapo uhakika wa Taasisi za Umma kupata magari kwa urahisi kwa sababu fedha za ununuzi wa magari zitakuwa zimetengwa maalum “ring-fenced”.



### 3.0 FAIDA ZA MFUMO WA UNUNUZI WA PAMOJA WA MAGARI YA SERIKALI:

Mfumo wa Ununuzi wa pamoja wa magari ya Serikali toka kwa watengenezaji una faida zifuatazo:-

- Kupungua kwa gharama za mchakato wa zabuni ambao unahusisha matangazo, karatasi, muda pamoja na mawasiliano.
- Punguzo la bei linalotokana na ununuzi wa idadi kubwa ya magari (trade discount) pamoja na
- Punguzo la bei linalotokana na mzabuni kulipwa kwa wakati (cash discount).

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:  
Mtendaji Mkuu

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA)

Mtaa wa Bohari na Barabara ya Nyerere,

Eneo la Keko Mwanga,

SL.P 9150,

Dar es Salaam

Simu: +255 22 286 6071/286 1617

Nukushi: +255 22 286 6072

Tovuti: [www.gpsa.go.tz](http://www.gpsa.go.tz)

Barua pepe: ceo@gpsa.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI**  
**SERIKALINI**



**MFUMO WA UNUNUZI**  
**WA PAMOJA WA**  
**MAGARI YA SERIKALI**

# UTANGULIZI

Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya 2011 katika kifungu Na. 50 kinaelekeza Taasisi za Umma kutumia mfumo wa ununuzi wa pamoja wa Vifaa na Huduma Mtambuka yakiwemo magari. Aidha kanuni Na. 131 (4) (a) ya Ununuzi wa Umma (GN446) pamoja na waraka wa hazina na. 3 wa mwaka 2014/15 zinaelekeza taasisi zote kuwasilisha kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) mahitaji yao ya vifaa na Huduma Mtambuka ili kufanyiwa Ununuzi wa Pamoja.

Katika kutekeleza jukumu hili, Wakala umeandaa utaratibu juu ya kutekeleza mfumo wa ununuzi wa pamoja wa magari ya Serikali kwa kuzingatia matakwa ya sheria. Aidha utaratibu huu unahusisha pia magari yanayohitajika katika Balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali ambapo mahitaji yote yatapelekwa kwa Mtengenezaji/Muuzaji na kuelekezwa sehemu ambapo atapeleka magari hayo. Utaratibu wa mfumo huu ni kama ifuatavyo:



- i. Ununuzi wa pamoja wa magari ya Serikali utafanyika kutoka kwa watengenezaji.
- ii. Mahitaji ya ununuzi wa magari kwa taasisi zote za umma yatawasilishwa GPSA kwa wakati mmoja wakati wa maandalizi ya bajeti na fedha za kununulia magari ya Taasisi zitatengwa na kutunzwa kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango.
- iii. Kwa vile bei za magari hutokana na viwango vya kubadilisha fedha za kigeni ambazo hubadilika kwa sababu za kiuchumi, mabadiliko hayo yanaweza kuongeza au kupunguza bei za magari kwa mujibu wa sarafu ya Tanzania.
- iv. Msawazisho wa magari (standardization) utafanywa na Wizara ya Ujenzi kuonesha aina ya magari ya kununuliwa.
- v. Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaainisha stahili za maafisa watakoatumia magari.



## 2.0 UTEKELEZAJI WA MFUMO WA UNUNUZI WA PAMOJA WA MAGARI YA SERIKALI

- i. Taasisi zinapaswa kupata kibali cha ununuzi wa magari kutoka kwa Mh. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwasilisha nakala za kibali hicho kwa Mtendaji Mkuu, GPSA.
- ii. Maafisa Masuuli ambao mafungu yao yametenga bajeti za ununuzi wa magari wanatakiwa kuwasilisha maombi ya ununuzi huo GPSA na nakala za barua kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango zikifafanua idadi, hadhi ya mtumiaji na aina (specifications) ya gari husika
- iii. Maafisa Masuuli wataandika barua pamoja na fomu za kufanya uhamisho wa fedha za ununuzi wa magari hayo kutoka kwenye mafungu yao na kuzipeleka Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango ili zihamishiwe GPSA. Utaratibu huu hautahusu mafungu ambayo hayategemei ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.
- iv. Kwa mafungu ambayo yametenga bajeti za ununuzi wa magari kutokana na fedha zao za ndani au yasiyotegemea ruzuku ya Serikali, yafanye uhamisho wa fedha zinazo stahili kwa kuzipeleka moja kwa moja kwenye akaunti Na. 9925262591 (inayotumia Tshs) kwa jina la GPSA – UNUNUZI WA MAGARI KWA PAMOJA COLLECTION ACCOUNT iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

AU